

# Maigizo katika fasihi simulizi: mfano wa kirarire katika nyimbo za tohara za wameru

Mutegi, Lewis

## Abstract:

Mada ya utafiti huu m maigizo katika fasihi simulizi kwa kurej elea mifano kutoka kirarire katika nyimbo za tohara za Wameru. Mtafiti ameangazia umuhimu wa maigizo katika utanzu huu wa nyimbo kwa lengo la kudhihirisha jinsi ambavyo wahusika katika nyimbo hizi huwasilisha ujumbe wao kwa njia ya ubunifu. Mtafiti pia alinua kuwaonyesha baadhi ya watafiti wa awali ambao hushikilia kuwa hakuna maigizo katika bara la Afrika kwamba kweli yapo. Utafiti huu uliongozwa na Nadhariaya Maigizo ambayo husisitiza umuhimu wa kuonyesha mitagusano ya wanajamii katika maisha yao halisi kupitia vitendo vya jukwaani. Nadharia hii pia huonyesha umuhimu wa hadhira katika kuwatathmini waigizaji wanapoendelea na vitendo vyao jukwaani. Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi wa tasnifu. Hapa, mtafiti ameifafanua mada ya utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo wa utafiti. Udurusu wa maandishi pamoja na nadharia iliyoongoza utafiti pia zimefafanuliwa. Mbinu za utafiti zilizotumiwa katika utafiti huu zimefafanuliwa. Sura ya pili inaangazia historia ya jamii ya Wameru ambao ndio watafitiwa. Mtafiti amefafanua mifumo ya kisiasa na kijamii ya Wameru, fasihi simulizi na utamaduni wao pamoja na vipawa vyao vya kisanii. Lengo kuu hapa ni kudhihirisha kuwa ingawa bara la Afrika limepitia mabadiliko makubwa ya kitamaduni, bado kuna jamii ambazo zingali zinathamini utamaduni wake. Sura ya tatu inachunguza sifa za maigizo katika kirarire. Baadhi ya yaliyoshughulikiwa ni njia ya mawasiliano, jukwaa, tukio la kuigizwa, mila na utamaduni zinazohusika na ujumi na itiksadi ya mawasiliano katika kirarire. Sura ya mwisho inatoa muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo ya utafiti. Hatimaye kuna marejeleo ya utafiti huu.